AFRIKA

# TWENDE

Kulitia moyo kanisa katika ulimwengu wa umisheni

Sehemu ya 4, Toleo la 2



Nini kusudi la biashara?


Wakristo wafungua biashara Afrika Magharibi

Mungu hakutengeneza meza, aliumba miti

## BIASHARA YA KIMISHENI

### gundua tena kufikiri kibiblia kuhusu utajiri, biashara na umisheni

# YALIYOMO











## 03 Maoni ya Mhariri

## 04 MUNGU HAKUTENGENEZA MEZA, ALIUMBA MITI

Hadithi ya Msamaria Mwema inaweza kusaidiaje biashara ya kimisheni? Mfanyabiashara Mghana, Johnson Asare, kwa miongo mitatu ameonyesha jinsi umisheni na ujasiriamali vinavyoweza kukamilishana na kuimarishana.

## 06 NJOO UTUSAIDIE

Ni nani bora zaidi wa kuifikia Afrika ya Kaskazini ambayo wakazi wake wengi ni Waislamu zaidi kuliko Wakristo walioko Afrika ya Kusini? Soma jinsi viongozi wa kanisa katika Afrika Kaskazini wanavyoungana na makanisa ya kusini mwa Sahara kuwapokea wafanyabiashara kama wamishonari.

## 08 NINI KUSUDI LA BIASHARA?

Afisa Mtendaji Mkuu, Septi Bukula, anajadili kwa nini wamishonari na wafanyabiashara wanaishi katika ulimwengu tofauti, na jinsi mtengano huu unavyozuia fursa kubwa kwa kazi za misheni.

## 10 NENDA! Habari za kuhamasisha kanisa katika Afrika

## 12 Makundi ya Watu: WAGUJARATI


© 2019 AFRIGO.

**AFRIKA TWENDE** ni chapisho lenye lengo la kuleta ufahamu, uhamasishaji, mafunzo na kusajilisha kanisa na mtu mmoja mmoja katika Afrika kwa nia ya kujihusisha na umisheni duniani.

**Msanifu:** Pilgrim Communications

Maoni yaliyoelezwa katika makala za Gazeti hili siyo lazima yawe ya Mchapishaji.

Picha halisi hutumika inapobidi. Majina hutumika kwa sababu za kiusalama.



Picha: Kehinde Ojo

# WAJIBU WA BIASHARA KATIKA UMISHENI

Kuna hadithi moja inayohusu kundi la watu walioishi karibu na pwani. Baada ya miaka kadhaa wakishuhudia ajali za kuzama kwa meli baharini na matokeo yake ni kupotea kwa maisha ya watu na mali, waliamua kufanya jambo fulani kuhusu hali hiyo. Walijenga kibanda karibu na pwani kwa ajili ya kuwahifadhi waathirika wa ajali hizo. Mtu mmoja alitoa wazo la kuweka pia mgahawa ili kuwasaidia wale waliokuwa wanaokolewa kupata chakula na vinywaji kwa urahisi. Kwa vile ajali za meli hazitokei mara kwa mara, kulitokea wazo la kuuza vitafunwa pamoja na vinywaji kwa wateja wengine wakati hakuna ajali ya meli. Hivyo biashara ilikua vizuri. Walakini, ilipotokea ajali ya meli, hakuna mtu aliyejali kama kuna ajali ya meli imetokea! Kwa hiyo kusudi la mwanzo la kuanzisha kibanda kwa ajili ya waathirika wa ajali za meli likawa limeshindikana.

Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, "fanyeni biashara hata nitakapokuja" (Luka 19:13).

Katika masimulizi kutoka kitabu cha Luka, maelekezo ya Bwana mkubwa kwa watumishi wake yaliwataka watumie pesa alizowapa kufanyia biashara mpaka atakaporudi. Kwa hiyo, kitu muhimu kabisa walichotakiwa kufanya wale watumishi ni kuwekeza zile pesa katika biashara wakati wanamsubiri bwana wao. Motisha ya kufaulu katika biashara hii ilikuwa ni kumfurahisha bwana wao kwa kupata faida atakaporudi. Hivyo, maana ya biashara siyo tamaa ya watumishi kufanya watakacho, bali furaha ya bwana wao kupata faida ya pesa zake. Basi, siyo biashara kama biashara tu, bali biashara kama kazi kamilifu katika mtazamo wa bwana wao.

Ni katika ufahamu huu ndipo akili zetu sisi Wakristo zinapowekwa huru kutumia biashara au kazi mbalimbali nchini mwetu au kutoka nje ya nchi kama zana za utumishi. Kiuhalisia, maswali ambayo Wakristo wafanyabiashara wanapaswa kumuuliza Mungu, ni haya, 'Ni nini unataka nifanye ni timize kwa ajili yako kupitia biashara hii? Na, 'Ni kwa namna gani biashara hii inatakiwa ikutumikie pamoja na kusudi lako?' Suala moja kubwa tunalopaswa kulitatua haraka katika shughuli zetu tofauti tofauti , na hata katika maeneo mengi ya maisha yetu, ni suala la umiliki. Ni nani ananimiliki mimi? Ni nani anamiliki biashara yangu? Ni nani anamiliki taaluma yangu? Ni nani anamiliki rasilimali zangu ambazo zimewekwa chini ya uangalizi wangu?

Katika toleo hili, utajifunza jinsi Mungu anavyofanya kazi huko Afrika Kaskazini akitumia biashara na elimu kuwaunganisha wenyeji kupitia mkakati wa "Nenda Kaskazini". Utasoma simulizi za kushangaza kuhusu uaminifu wa Mungu katika maisha ya Mchungaji Johnson Asare, msomi, mmishonari na mfanyabiashara, na katika maisha ya Bwana Septi Bukula, kiongozi wa umisheni na mfanyabiashara. Utafahamu jinsi hadithi ya Msamaria Mwema, kama ilivyotumiwa na Mchungaji Asare ilivyosaidia ufahamu wake wa kibiashara na kazi ya umisheni. Ndugu Bukula anashirikisha ufahamu wake juu ya masomo aliyojifunza kutoka kwa baba yake kuhusu kufanya kwa pamoja biashara na umisheni, ukilinganisha na yale mahubiri yaliyokuwa yanaenezwa na makanisa yakikatisha tamaa kwa kudai kuwa Wakrsito wanatakiwa kupokea baraka lakini hawahusiki kutumia utajiri wao kwa ajili ya watu wengine.

Ni shauku yangu kuwa toleo hili litafungua macho yako kuona fursa nyingi zilizoko katika ulimwengu wa umisheni, na hasa katika eneo la biashara, na Mungu atakutumia wewe pamoja na mazingira yako kushawishi wengine katika kupunguza pengo kati ya biashara na umisheni.

*Kehinde Ojo ni Mkurugenzi wa Programu ya Mpango wa Kusaidia Maendeleo ya Wenyeji. Michango yake ya awali kwa AfriGO ni pamoja na 'Kupalilia Roho ya Ukarimu' (sehemu ya 1 toleo la 4). Wasiliana naye kwenye: kehinde.ojo@ifeworld.org.*



# MUNGU HAKUTENGENEZA MEZA; ALIUMBA MITI

Na MERCY KAMBURA

Kuna uhusiano gani kati ya hadithi ya Msamaria Mwema na Biashara ya Kimisheni? Au biashara yo yote kwa ujumla? Johnson Asare, mwanzilishi na Mkurugenzi wa kitaifa wa huduma za Markaz Al Biashara huko Tamale, Ghana, anatoa funzo la kutufungua macho kwa kutumia hadithi ya Msamaria Mwema kuhusu mahitaji ya Mkristo katika kufanya biashara na umisheni kwa mafanikio.

Johnson ambaye hupenda kujiita mtumishi mkuu wa huduma, anajua vizuri umuhimu wa biashara na umisheni. Kabla ya kuingia katika huduma, Johnson alikuwa mwalimu wa sayansi, na aliongozwa kumpokea Yesu Kristo na mishonari kutoka shirika la SIM, na amekuwa kwenye kazi za misheni kwa miaka 30. Hivi leo, yeye ni mhadhiri wa masomo ya Biashara ya Kimisheni katika vyuo. Pia kwa sasa anamalizia shahada yake ya Uzamivu katika Imani, Kazi na Uchumi katika Seminari ya Asbury Jimbo la Kentucky nchini Marekani.

Kwa Johnson, kila kitu ni kitakatifu katika Bwana. Na huu ndio mtazamo ambao ulimwezesha kuanzisha huduma ya Markaz Al Bishara, ambayo maana yake ni 'Kituo cha Habari Njema'. Kupitia miradi 28 iliyokusudiwa kueneza Injili na mingine kuanzilishwe, huduma hii kwa kweli ni mfano bora zaidi wa kuendesha kazi ya biashara na umisheni kuwa pamoja.

Kituo cha Markaz Al Bishara hutoa huduma za kambi za watoto, huchimba visima vya maji, huhubiri Injili kwa njia ya redio, na hutoa mikopo midogo midogo kwa watu ili kuanzisha biashara zao. Pia kituo kimejitosa katika huduma za kusaidia watu waliopatikana na majanga mbalimbali na hujenga nyumba za bei naf uu kwa jamii za vijijini. Nyumba zaidi ya 220 za bei nafuu tayari zimeshajengwa. Yeye akiwa msomi, Asare ameanzisha Chuo cha Afrika kinachotoa mafunzo mara mbili kwa mwaka kwa waanzilishi wa makanisa na wafanyakazi kutoka nchi 30 za Afrika.

Markaz Al Bishara ina idara kubwa ya kusimamia kituo cha malazi na mikutano cha Radach chenye uwezo wa kuchukua watu zaidi ya 500,000 kila mwaka kwa mikutano mbalimbali. Zaidi ya asilimia 90 ya wageni wanaotumia Kituo hiki huwa siyo wa imani ya kikristo. Kituo cha malazi na mikutano cha Radach ni rasilimali ambayo inategemeza shughuli za huduma kifedha kwa asilimia 90.

Akiwa amefanya kazi sambamba na SIM kwa miaka 30, Johnson ni kijito kinachobubujisha hekima na kicheko. "Nimefanya makosa mengi, na makosa hayo yamenipa uzoefu mwingi. Mungu ametumia makosa yangu kufanya vitu vingi," anasema Johnson.

Miaka 25 iliyopita, Johnson alishirikisha wazo la kuanzisha mradi ambao ungesaidia kuzalisha pesa za kuendesha umisheni. Wakati huo, wazo hilo halikuonekana kama ni wazo lenye manufaa kwa huduma. Kwa hiyo, alijitolea yeye mwenyewe kulifanyia kazi wazo hilo. Alianzisha biashara ndogo ndogo ili kupata mtaji kwa mtaji kwa mradi mkubwa; akaanza kununua na kuuza mchele, njugu na nafaka zingine.

Pia Wakristo wengi wenyeji walisaidia kupata asilimia 75 ya pesa za kuanza mradi ambao ungeweza kutegemeza kazi ya Injili. Kati ya dola milioni 2 zilizokuwa zinahitajika, Johnson aliweza kukusanya dola 500,000 kama msaada kutoka nje; na dola milioni 1.5 zilikusanywa kutoka ndani ya nchi.



## Mafunzo kutoka Msamaria Mwema

Wakati Johnson alipokuwa anasikia kwa nguvu msukumo wa ndani wa kufanya biashara kwa kusudi la kusaidia kueneza injili, mfano wa Msamaria Mwema ulizungumza naye kwa sauti kubwa kutoka ndani ya moyo wake. Kutokana na mfano huu, Johnson alipata tabia/sifa nne za Msamaria Mwema zilizomfanya awe mfano kamili katika kuelezea upendo.

1. **Huruma:** Msamaria Mwema alikuwa na huruma. Miongoni mwa watu wote waliopita alipokuwa yule mtu aliyekuwa amepigwa na wanyang'anyi na kuachwa akiwa mahututi, ni Msamaria Mwema pekee ndiye aliyekuwa na huruma ya kumsaidia.
2. **Uwezo wa kutenda:** Msamaria Mwema alikuwa na uwezo wa kufanikisha mambo yake. Aliweza kumpa huduma ya kwanza kwa kumsafisha na kumfunga vidonda na kuifanya hali yake iwe imara kiasi cha kuendelea na safari mpaka alipomfikisha kwenye nyumba ya wageni.
3. **Uwezo wa kiuchumi:** Msamaria Mwema alikuwa na fedha za kumlipa mtunza nyumba ya wageni, na kuahidi kuwa angekuja kulipa madeni yote ambayo yangesalia katika kumhudumia yule mjeruhiwa.
4. **Ujasiri:** Msamaria Mwema alikuwa jasiri kiasi cha kusimama na kumsaidia Myahudi. Tendo hilo ni ajabu kwa maana Wasamaria na Wayahudi huwa wanachukiana.

Kati ya tabia/sifa hizi nne, Johnson aliona wamishonari wengi wanapungukiwa na sifa ya tatu – uwezo wa kiuchumi. Na Johnson alitafuta kuondoa upungufu huu kwa kutumia kila alichokuwa nacho. Ulemavu huu wa kiuchumi ndio ambao umefanya mashirika mengi ya kimisheni kutegemea sana msaada kutoka nchi za nje. Matokeo yake, mashirika mengi yamekufa kwa haraka sana. Johnson alihitaji kufanya

jambo la asili na ambalo lingetokana na mazingira ya nyumbani na ambalo lingekuwa endelevu.

"Afrika inaweza kufanya kile kinachofanywa na nchi za Magharibi. Tumetegemea nchi za Magharibi kwa muda mrefu; tunahitaji kuhifadhi utu wetu" anasema Johnson.

Ukilinganisha kuenea kwa Ukristo na Uislamu katika nchi ya Ghana ndiko kulimfungua macho Johnson. Anaelezea jinsi walimu wa Kiislamu walivyokuja Ghana kama wafanyabiashara miaka 450 iliyopita. Walifanya biashara ya kola, pilipili, chumvi na dhahabu kwenye ukanda wa Volta. Walitajirika na mwishowe wakawa washauri wa machifu.

Wakristo, kwa upande mwingine, walifika sehemu ya kusini mwa Ghana wakiwa na pesa kutoka Magharibi, mwisho wake wakasababisha utegemezi. Zaidi ya asilimia 95 ya mashirika yaliyotegemea ufadhili kutoka ng'ambo yalikufa. 'Zalisha pesa zako mwenyewe na pesa hizo zitaongezeka', anashauri Johnson. 'Maendeleo ni polepole; nenda hatua kwa hatua, na Mungu atakubariki'.

Upendo wa Mungu unaweza kuenezwa kwa njia nyingi, mara nyingi bila maneno. Ikiwa na wafanyakazi 168, na wafanyakazi wa kujitolea zaidi ya 300 huko Tamale, katika moja ya majimbo maskini zaidi ya nchini Ghana, huduma inaeneza upendo wa Kristo kama moto wa mwituni wa Australia.

Kwa Johnson, kazi ni kitendo cha ibada.

"Mimi ni mkulima, mchungaji, mfanyabiashara, na mwandishi. Mungu ndiye sababu ya kila kitu ninachofanya. Hakuna kazi takatifu na hakuna kazi ya kidunia. Kila kitu ni kitakatifu kwa Bwana. Biashara ni tendo la ibada," anasema Johnson. Tusitenganishe imani na biashara. Tunatakiwa kuviweka vyote pamoja na kutafuta njia za kuzifanya zikamilishane.

"Mungu hakuumba meza", anasema Johnson. "Mungu aliumba miti. Mungu anataka sisi tutumie bongo zetu."

*Mchungaji Johnson Asare ni mkurugenzi wa kituo cha mikutano cha Radach, Tamale,Ghana (www.radach.org). Ni mwanzilishi na mkurugenzi wa kitaifa wa huduma za Markaz Al Bishara (www.bisharapraise.radach.org) . Ameandika vitabu na ni mnenaji wa masuala ya Biashara ya Kimisheni. Unaweza kuwasilina naya kwa: Johnson@radach.org.*

# BIASHARA YA KIMISHENI NI NINI?

**Biashara za Kimisheni (BK) ni** kazi za kibiashara za wakristo wakiwa na nia ya kutumia biashara hizo kufanya kazi za misheni. Wamishonari wanaojihusisha na biashara za kimisheni wameitwa na Mungu na kutumwa na kanisa kushirikisha watu wengi injili ya Kristo na kuwafanya watu kuwa wanafunzi katika tamaduni zote, wakitumia stadi zao za biashara. Makundi ya aina kadhaa za BK yana msisitizo tofauti tofauti, lakini yote yanatumika kwa ajili ya kazi za umisheni.

## 1. Biashara kama Umisheni

"Business as Mission" (BAM) inahusiana na biashara inayotumika kama ukumbi halisi wa huduma. Hawa wahudumu wa kimisheni wanatumia mawasiliano kupitia michakato ya kawaida ya kufanya biashara, kama vile waajiriwa, wasambazaji wa vifaa, wateja, wafanyakazi wa serikali na washirika wa biashara. Biashara hii hufuata mifano ya kanuni za kibibilia na huleta amani (shalom) kwa jamii ya wenyeji.

## 2. Biashara kwa ajili ya Mabadiliko

"Business for Transformation" (B4T) ni aina ya biashara ambazo zimewekwa kimkakati katika maeneo ambapo Kristo hajulikani au anajulikana kwa kiasi kidogo. Zimeundwa kubuni ajira, nia ikiwa ni kuleta mabadiliko katika sehemu ya jamii, na hasa kupitia uinjilisti, ufuasi na uanzilishi wa makanisa.

## 3. Biashara yenye malengo ya Umisheni

"Business- based mission" (BBM) inamaanisha aina ya biashara inayotumika kama njia kwa wamishonari kufanya kazi ya umisheni katika nchi. Pale ambapo biashara inafanikiwa, inaweza kulipa sehemu au mishahara yote ya mishonari. Kimsingi kusudi la huduma ni nje ya biashara, ingawa baadhi ya huduma zinaweza pia kuchanganya biashara na huduma. Kazi ya kutengeneza mahema kama ile iliyokuwa inafanywa na Mtume Paulo ni moja ya ina za BBM.

## 4. Biashara kwa ajili ya umisheni

"Business for Mission" (BFM) ni miradi yenye kusudi la msingi la kutengeneza faida ili kusaidia kazi za misheni. Kama BFM, matumizi ya faida inayotarajiwa lazima ielezwe na kutengwa kwa ajili hiyo katika mwanzo wa kuanza shughuli za biashara husika. Mifano inaweza kuwa kama vile kuwa na Kampuni ya kusafirisha watalii ambayo inaweza kuwa inatoa tiketi maalum kwa ajili ya wamishonari au kuwa na kampuni ya uchapishaji ambayo ni maalum kwa ajili ya kuchapisha nakala kwa matumizi ya kazi za misheni.

## 5. Taasisi ndogo za Fedha

Taasisi ndogo za kifedha hutoa mikopo midogo kwa mtu mmoja binafsi au kwa makundi ili kuwasaidia kuanza biashara ndogo ndogo. Taasisi hizi zinafaa sana kwa jamii maskini zaidi, mahali ambapo fursa za ajira ni haba. Shirika linalotoa mitaji pia hutoa mafunzo kwa wapokeaji wa mikopo na husimamia utaratibu mzima wa mikopo. Maneno kama taasisi za kukopesha, biashara ndogo ndogo au ujasirimali mara nyingi hutumika kumaanisha taasisi zinazotoa mikopo midogo midogo.

# 'NJOO HUKU UTUSAIDIE'



Ni nani bora zaidi kuwafikia Waislamu wa Afrika isipokuwa Wakristo wa maeneo mengine ya Afrika? Hayo ndiyo yaliyokuwa mawazo ya mwaka wa 2011 wakati wa Mkutano wa Vuguvugu la Mkakati wa Mataifa ya Afrika (MANI), ambalo lilizalisha kwa mkakati wa Nenda Kaskazini*.

Asilimia 63 ya Waafrika wanaoishi kusini mwa Sahara wanajitambulisha kama Wakristo, ilhali zaidi ya asilimia 90 ya Afrika Kaskazini ni Waislamu. Mamilioni ya Wakristo kwa wastani wanaishi kwa amani Kusini, lakini wachache walioko Kaskazini wako kwenye adha na mateso. Katika Matendo ya Mitume 16:9, mtu mmoja kutoka Makedonia alionekana kwa ndoto akimsihi Mtume Paulo kwa kusema, 'Njoo huku utusaidie'!. Vivyo hivyo, yanaashiria mateso wanayopata Wakristo wa Afrika ya Kaskazini.

Mkakati wa Nenda Kaskazini ulitokana na wazo kwamba Waafrika wana sifa ya pekee kuwahudumia ndugu zao katika sehemu zingine za bara la Afrika. Wakristo wanaoishi katika Afrika ya Kaskazini walilipokea wazo hili na mwaka 2015, Mshikamano wa kutoka Kusini kuelekea Afrika Kaskazini Nenda Kaskazini ulizinduliwa. Huku viongozi wa makanisa kutoka Kaskazini wakianzisha mahusiano na mashirika na makanisa ya Kusini, ili kuweza kuwaleta pamoja wafanyakazi walioko katika nchi za sehemu ya Kusini mwa Sahara.



Mchungaji Yohana, kutoka Afrika ya Kusini, yuko katika timu ya uongozi wa Nenda Kaskazini na Kanisa la Afrika ya Kaskazini. Anasema, 'Tunaishi kana kwamba baadhi ya milango imefungwa kwa Mungu. Tumeunda misemo kama vile, "nchi zilizofungwa", badala ya kutaja tu makundi ya watu ambayo bado yanakosa Injili. Kwa mwitikio, Nenda Kaskazini ina maono ya kutupa changamoto na kubadilisha namna tunavyofikiri na kutendea kazi yetu... Kwa sababu hii, tunasema, "Njoo uone!"

Malengo ya Nenda Kaskazini ni ya aina mbili: Kwanza, ni kuwatia moyo Wakristo kutoka Kusini kwenda kuishi Kaskazini, wakiendesha biashara zenye mlengo wa uenezaji wa injili ili waweze kujitegemeza wenyewe. Hawa wajasiriamali wanatumwa na makanisa yao ya nyumbani kwenda kwenye makanisa yaliyowapokea. Makanisa yale huwasaidia kupata makazi katika jamii na kuwapa mkono wa ushirika na kuwatia moyo ili waweze kuishi katika jamii za huko Kaskazini. Kanisa linalowatuma huwapa msaada wa kifedha kwa kadiri inavyohitajika, pamoja na kuwategemeza kwa maombi na kuendelea kuwatia moyo kutokana na kuwa wako mbali nao.

Lengo la pili ya mwelekeo wa Nenda Kaskazini, ni kuwatia moyo wanafunzi wa vyuo vikuu kutoka Kusini kwenda kusoma katika Vyuo Vikuu vilivyoko Kaskazini, mahali ambapo wanaweza kuwafikia watu walio karibu na vyuo hivyo kwa njia ya ushuhuda wa imani yao. Kwa pamoja, wafanyabiashara na wanafunzi wanategemewa kuishi mtindo wa maisha ya kikristo, huku wakiendelea kuwa sehemu mpya ya jamii ya Kaskazini.

Mkakati wa Nenda Kaskazini una wanachama kutoka Mashariki, Magharibi, Kati, na Kusini mwa Afrika, ikiwa ni pamoja na ndugu kutoka mabara mengine katika kuunga mkono mkakati huu. Hadi leo, wengi wa wale ambao tayari wameshatumwa kwenda Kaskazini, wanatoka nchi za Afrika Magharibi kutokana na faida



waliyonayo ya kuzungumza lugha ya Kifaransa, ambayo ndiyo lugha inayohitajika huko Afrika Kaskazini. Kila Mkristo mfanyakazi huungana na kanisa lililopo huko, na hasa wajibu wao siyo kuanzisha makanisa mapya, bali kumshuhudia Kristo katika jamii zao mpya na kushika mkono Kanisa la huko Afrika ya Kaskazini.

Mike ni Mkurugenzi Mtendaji wa Ushirika mwingine kule Kusini na ambaye ndiye sauti inayoongoza katika mkakati huo wa Nenda Kaskazini, anasema,

*Kwa nini Mungu aweke Wakristo zaidi ya milioni 40 kutoka makanisa ya Kiinjili katika sehemu ya kusini mwa Sahara ya Afrika, akiwa amewawezesha kuwa na uongozi wenye uwezo na rasilimali zinazoweza kufikia Afrika yote na ulimwengu na Injili? Kwa nini Mungu aweke rasilimali hiyo kubwa mno ya watu karibu kabisa na watu wenye mahitaji, ambao ni Waislamu waliofikiwa kidogo huko maeneo hayo? Mungu ana ajenda kwa ajili ya kanisa la sehemu ya kusini mwa Sahara na hata huko ughaibuni ambapo wapo Waafrika wanaoweza kutimiza wajibu muhimu katika hatua ya mwisho ya kupeleka Injili Kaskazini na kwa mataifa mengine ambayo bado hayajafikiwa na Injili'.*

Mkakati wa Nenda Kaskazini pia unasaidia Wakristo Waafrika ambao wamepoteza kazi kwa sababu ya imani yao katika Kristo Yesu. Mateso kwa Wakristo yanaendelea katika maeneo mengi; na usalama kwa Wakristo bado ni jambo kubwa la kuzingatia. Na kwa kweli bado ni hatari na kamwe si vema kuchapisha au kuwatambulisha wafanyakazi au Wakristo wenyeji kwa ajili ya usalama wao. Ingawa hatutakiwi kuishi na roho ya woga (2 Tim. 1:7), hatutaki kutoa fursa kwa wale ambao ni maadui wa Injili kutotuelewa.

Licha na masuala haya ya usalama, Nenda Kaskazini imetengeneza utaratibu unaoitwa Uzoefu wa "Njoo uone". Hii ni safari fupi ambayo hufanyika kila mwaka kule Kaskazini na ni kwa ajili ya wachungaji na viongozi kutoka Kusini mwa Sahara, na mtu yeyote anayependa kazi ya injili kuja na kujionea kinachoendelea na nini kinahitajika huko Kaskazini. Safari za kutembelea maeneo ya kihistoria hutufanya kuona na kutambua kuwa Afrika Kaskazini ina utajiri mkubwa wa historia ya Ukristo, kitu ambacho kimefunikwa na kusahaulika kwa sehemu kubwa.

Richard, ambaye ni raia wa Afrika Kusini aliyeko kwenye timu ya Nenda Kaskazini alihojiwa kwa ajili ya makala haya, naye analisihi Kanisa la Afrika 'kutafuta uhalisia juu ya maisha ya kikristo- na siyo tu kufikiria jamii yako mwenyewe. Fikiria juu ya wale wanaoishi maeneo ambayo kuwa mkristo ni sawa na kukabiliana na matatizo makubwa yasiyoelezeka. Unapaswa kujua nini kinahitajika kusaidia sehemu zingine za ulimwengu'.

Wakristo walioko Kusini mwa Sahara kwa kweli wanasikia wito kutoka Kaskazini wa, 'Njoo huku utusaidie'! Na wanauitikia wito huo.

Kuna Wakristo huko Kaskazini, lakini ni wachache. Wanahitaji ndugu kuja na kusimama pamoja nao. Kama unapenda kujifunza zaidi kuhusu hatua inayofuata juu ya Uzoefu wa "Njoo uone", au kujihusisha kwa njia nyingine na Nenda Kaskazini, tafadhali tuandikie kwa: info@maniafrica.com.

# WALIOITWA: SEPTI BUKULA



Picha: Timothy Coleman

## Kusudi la biashara ni nini?

Nilipoulizwa swali hili yapata miaka 14 iliyopita, nilifikiri nilijua Jibu lake. Wakati huo nilikuwa nahudhuria kongamano huko Jakarta nchini Indonesia, pamoja na waumini kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni. Baada ya juma moja la majadiliano, hatimaye tulikuja kufikia hitimisho moja: kusudi la biashara ni kumtukuza Mungu.


Huo ulikuwa ni mwanzo wa safari. Swali lililofuata lilikuwa: Je, biashara inayomtukuza Mungu inatofautiana vipi na biashara ambayo haitafuti kumtukuza Mungu? Imenichukua miaka kadhaa kufikia mahali pa kupata baadhi tu ya majibu.

Baada ya majibu hayo, nilipata mwanzo wenye nguvu katika biashara na huduma, miaka mingi kabla ya kupata maneno haya, Biashara Kimisheni (Missional Business, MB) kuundwa. Baba yangu alikuwa mtu wa ajabu – mtu pekee aliyekuwa mchungaji muda wote, mfanyabiashara muda wote na mkulima muda wote. Hivyo ndivyo alivyolea watoto wake wanane. Yeye na mama yangu waliongoza makanisa 20 ya mtaa katika mtindo wa zamu. Kwa sababu kwa hakika tunaweza kusema walikuwa hawalipwi, ilibidi watafute namna ya kuhakikisha familia inapata chakula. Baba yangu aliniambia, 'Mwanangu, situmii pesa ya kanisa kuendesha familia yangu; bali ninatumia pesa ya familia yangu kuendesha kanisa'.

Shughuli za baba yangu zilizidi hata chakula cha kujikimu; alikuza mahindi, na alikuwa na mifugo, lakini kwa kiwango kidogo tu cha kibiashara. Kama watoto, kila mmoja wetu alipewa

## BUSINESS AS MISSION

### BUSINESS IS GOD'S IDEA




Business has God-given power to do good in society by creating jobs, multiplying resources, driving innovation and catalyzing human flourishing.



### BUSINESS + THE CHURCH

If business is a God-given calling, then it is a necessary component of the church to reach the world for Christ.

### GOD CALLS BUSINESS PEOPLE FOR CREATIVE SOLUTIONS




**BUSINESS FIGHTS POVERTY**

One billion people were lifted out of poverty in the 20 years between 1990 and 2010; two thirds of that lift is attributed to capitalism and free trade rather than governments and NGOs.

**BUSINESS CREATES JOBS FIGHTS UNEMPLOYMENT**

Small and Medium Enterprises (SMEs) provide two-thirds of all formal jobs in developing countries in Africa, Asia and Latin America, and 80 % of jobs in low income countries.



### REDISCOVER BIBLICAL THINKING ABOUT BUSINESS

sehemu kubwa ya eneo na tuliwajibika kulima mazao ya biashara – kama vile kabichi, nyanya – huku tukifanya kila liwezekanalo ili kupata mavuno. Tuliuza mazao yetu kwenye masoko madogo mahali ambapo baba alikuwa anapajua. Tulimlipa mwenye nyumba kupata eneo la kuhifadhia mazao yetu. Baba yangu alihakikisha tunawajibika kwake kwa namna tulivyokuwa tunatumia pesa zetu.

Wakati wa mavuno, baba yangu aliweka sharti moja. Tulipaswa kufunga mfuko uliojaa mboga, kisha kununua sukari, majani ya chai, mafuta ya kupikia, na kupeleka mzingo wote huu kwa familia maskini. Hii ilikuwa ni kabla ya kujua utoaji zaka, wazazi wangu walinifundisha kuwa kama una vingi, unapaswa kuwapa wengine.

Injili ya Mafanikio imefanya uharibifu mkubwa kwa kuwafundisha watu kuwa Mungu yupo kwa ajili ya kuwabariki wao binafsi. Hii ni kinyume na mafundisho sahihi ya Biblia. Tunabarikiwa ili tueneze baraka kwa wengine! Kukabidhiwa na Mungu kwa baraka ni kukabidhiwa kwa kupewa wajibu wa kushirikisha baraka hiyo na wengine – siyo tu na familia yako au jamaa zako wa karibu, bali na jamii kubwa iliyobakia katika ufalme wa Mungu. Nawahimiza wafanyabiashara kujiuliza wao wenywe, "Je, naiona biashara yangu kama yangu tu, au kama biashara ya Mungu ambaye amenikabidhi kuiendesha?"

Sehemu kubwa ya ulimwengu wa biashara haijaunganishwa na kazi za umisheni. Biashara Kimisheni (MB) inabakia kuwa ni mazungumzo miongoni mwa jamii ndogo tu ya wafanyabiashara. Wamishonari na wafanyabiashara wanaishi katika sehemu mbili tofauti za dunia. Niliamua kuratibu tukio ambalo lilileta watu pamoja kutoka ulimwengu wa aina hizi mbili. Hivyo, huduma ya Injili ya Wekeza Afrika (Mission Invest Africa- MIA) ilifanyika mwaka 2018 huko Johannesburg, Afrika Kusini.

Kimakosa, wengi wanaamini kwamba biashara na Ufalme wa Mungu havichanganyiki, na hii inazuia fursa kubwa katika kuendeleza ufalme wa Mungu. Hali hii ya kutoelewana imesababishwa na makanisa ambayo yameweka utengano kati ya eneo takatifu na lile la kidunia. Watu wameaminishwa kuwa kufanya biashara siyo wito mkuu wa Mungu. Lakini vuguvugu la Biashara Kimisheni (MB) linaloshika mizizi leo linasahihisha upotofu huo.

Wengi wamefundishwa kwamba tunaweza kutenganisha shughuli zetu kwenye idara mbili tofauti, yaani 'idara yangu' na 'idara ya Mungu'. Biashara inaangukia chini ya 'idara yangu'. Tumeshindwa kuwafanya wafanyabiashara kuwa wanafunzi wenye mtazamo wa biashara kimisheni. Wamekua, hata katika makanisa yetu, wakifikiri kuwa biashara ni kwa ajili ya kupata utajiri tu. Kimaandiko, hii siyo kweli.

Kilicho kweli ni kwamba dunia na kila kilichopo ndani yake ni mali ya Bwana (Zaburi 24: 1). Hivyo, biashara ni mali ya Bwana. Kama unaendesha biashara, basi ni Mungu aliyekuweka hapo. Unashikilia sehemu hiyo ya ufalme kwa niaba yake.

Kwa hiyo, nini sasa unafikiria kuwa ndilo kusudi la biashara? Kama unakubali kuwa biashara ni kwa ajili ya kumletea Mungu utukufu, hiyo inamaanisha nini kwa biashara yako leo?

---

*Septi Bukula ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Hodhi ya Osiba (Osiba Holdings), ambayo hujishughulisha na maendeleo ya utafiti, ushauri na biashara utalii, ambayo ipo Johannesburg, Afrika Kusini.*
*Jiunge na Wekeza Umisheni Afrika.*
*https://www.facebook.com/www.missioninvestafrica.osiba.co.za/*

**WORKING TOGETHER FOR GOD 'S GLORY**

**BUSINESS FIGHTS HUMAN TRAFFICKING**

The International Labor Organization estimates that forced labor and human trafficking is a $150 billion industry worldwide. Economic vulnerability and a lack of dignified jobs is a leading cause of human trafficking.

**BUSINESS REACHES THE UNREACHED**

There are still 7000+ unreached people groups in the world. The majority of the unreached live where traditional missionaries can't go. Yet the world is open to business people who are able to have a long-term influential role in their communities.

**BUSINESS BUILDS RELATIONSHIPS**

The average person will spend 90,000 hours at work over a lifetime. People spend much of their waking lives in the workplace. The workplace is a key environment where we interact with others, build long-lasting relationships and are able to be a daily witness to the gospel.

**CALLS TO ACTION**

**AFFIRM**

We call upon the Church to affirm business as a God-given calling, and positively engage with leaders in church, business, missions and academia to influence attitudes towards business.

**RECEIVE**

We call upon business people globally to receive this affirmation and to consider how their gifts might be used to help meet the world's spiritual and physical needs.

**PRAY**

We call upon the global Church to pray for professionals to exercise their gifts effectively among all peoples and to the ends of the earth.

Lausanne
Business as Mission Network
www.lausanne.org/bam

Business is a God-given calling! Business people are able to use their gifts for God's glory and the common good, especially among the world's poorest and least-reached peoples.

# GO! NEWS OF AFRICA'S MOBILISING CHURCH

## Kusanyiko la Watumaji la Afrika Magharibi

"The West Africa Senders Gathering" lilikutana mjini Abidjan, Ivory Coast, somo kuu likiwa "Kuwaachia Wafanyakazi wa Afrika Magharibi kuingia kwenye Mavuno ya Mungu." Jumla ya washiriki 155 kutoka nchi 15, wakiwakilisha makanisa 77 na wakala wa kazi za umisheni waliwkutana kutoka tarehe 29 Oktoba hadi 2 Novemba 2018. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuwawezesha, kuwatia moyo, na kuleta ushirikiano miongoni mwa mashirika na watu binafsi kutoka Afrika Magharibi. Kusanyiko hilo liliimarisha nguvu za misheni na pia kubainisha fursa mpya na changamoto, na pia kuimarisha nguvu ambazo tayari mashirika ya kimisheni yalikuwa nazo.

Wajumbe wa kongamano hilo walikubaliana kwamba kanisa la Afrika Magharibi linalo wajibu wa kibiblia siyo tu wa kutuma wamishonari kutoka makanisa yao, bali pia wakuwasaidia vya kutosha wale wanaotoka kwenda kwenye kazi za umisheni. Ilipendekezwa kuwe na mabadiliko ya dhana yatakayo hakikisha usaidizi huo unatoka ndani ya mataifa ya Afrika. Mwisho wake, kongamano hili liliahidi kufanya kazi pamoja bila kujali mipaka ya kimadhehebu na uwakala katika kuendeleza ufalme wa Mungu katika nchi za Kaskazini na Kusini.


Nakala ya maazimio ya Kusanyiko hilo inapatikana kwa Kiingereza na Kifaransa kwa anwani hii: WAMO.Director@sim.org.



## Ilani ya Ukuzaji wa Utajiri

Mashauriano ya Kidunia juu ya 'Wajibu wa Ukuzaji wa Utajiri kwa Mabadiliko Kamili' yalifanyika nchini Thailand mwezi Machi 2017, na yaliratibiwa na Shirika la Lausanne na BAM Global. Washiriki walitoka kwenye sekta za biashara, Makanisa, huduma za kimisheni, taasisi za elimu, na wawakilishi kutoka mataifa 20, ambayo kwa pamoja waliandaa rasimu ya Ilani ya Ukuzaji Utajiri, ambayo ilijumuisha uthibitisho wa maandiko ya Biblia wenye vigezo 11 kuhusu ukuzaji wa utajiri. Unaweza kusoma Ilani hiyo kwenye hii Tovuti hapa chini.

https://www.lausanne.org/content/statement/wealth-creation-manifesto-bible-references




## MASHUA YA MBALI

Filamu hii muhimu inabainisha changamoto na thawabu za kazi ya misheni na inayaalika makanisa kukumbatia fursa zinazotokana nayo ili kuweza kuwafikia watu wanaoishi na kufa bila Kristo.

Katika hadithi ya Max, kijana wa mjini mkenya ambaye anaonekana ana kila kitu ambacho ni pamoja na: kazi ya ndoto yake, rafiki mzuri na msichana anayetarajia kumwoa. Kisha Max akutana na Yusef, Mwislamu ambaye ni mvuvi. Yeye na watu wake hawajui kanisa na wala hawana wakristo wa kuwashuhudia habari za Kristo. Kukutana kwao kunamfanya Max afikirie kama Mungu anamwita ili atumike kama mishonari.

Filamu inaibua vikwazo ambavyo lazima kuvishinda kama kanisa linataka "kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi" kwa kusisitiza kwamba inastahili kulipa gharama.

Mashua ya Mbali ni filamu inayopatikana kwa Kiswahili, Kiingereza na Kireno pia kwenye Tovuti hii: www.distantboat.com

## KIJIJI CHA BIASHARA

Kijiji cha Biashara au Venture Village (V2), ni Kituo cha Mafunzo kwa wale wanaotaka kuwa wamishonari ambao Mungu anawaita kufanya biashara na kazi ya umisheni pamoja. Kupitia V2, wajasiriamali hujiunga pamoja chini ya walimu, wakishirikiana na watu wengine ambao wanaanzisha biashara, na kustawi chini ya msaada wa makundi ya watu wa rika moja, washauri na wataalamu wa masomo – wote wakiungana kwa kusudi la kuwa na biashara zenye mlengo wa kumhubiri Kristo.

Mkakati huu wa V2 unaratibiwa kutoka Nairobi, Kenya; Lusaka Zambi; Abuja Nigeria, na unatoa kozi mbili, Accelerator na Boot camp (hizi ni aina za kozi). Kozi ya haraka (Accelerator) inatolewa ndani ya majuma 12 na inaleta pamoja kundi dogo la wanafunzi ambao ni wafanyabiashara wapya wapate mafunzo ya haraka lakini yanayotolewa kwa uangalifu mkubwa. Kila mtu anakuja na mpango biashara uliokamilika, ukiwa na malengo ya kila mwezi, na kupata nafasi ya kuwasilisha mpango biashara wake kwa wale wanaotegemewa kuwa wawekezaji. Ilhani Kozi fupi, inalenga kuboresha ujuzi walionao tayari wajasiriamali na kubadilisha mtazamo wao juu kuufanya ufalme wa Mungu kuwa na kishindo katika jamii.

Mkakati huu wa V2 umejengwa kutokana na tathmini, ushauri, mafunzo, ufadhili na msaada unaoendelea. Kiungo muhimu cha kuhusisha familia, imani na jamii inamaanisha kwamba wajasiriamali wanaotoka kijiji hiki watakuwa wameandaliwa vema kuungana na timu za wamishonari wenyeji au wale wa kutoka mataifa mengine duniani, wakileta upendo wa Kristo katika jamii ambazo hazijawahi kusikia. Nguvu yao katika kubadilisha maisha ya waajiriwa wao, wachuuzi na jamii zinazowazunguka kuhusu masuala ya kiroho, kijamii na kiuchumi inaelezewa vizuri na kwa matendo na maneno kutoka Mithali 11:10: " Wenye haki wasitawipo, mji hufurahi".

Ili kujifunza zaidi, juu ya mkakakti huu wa V2, tafadhali tembelea: www.venturevillage.org

## SIKU YA MAOMBI KWA WASIOFIKIWA ni tarehe Juni 19, 2020

Ni wapi watu wengi ambao bado hawajafikiwa na Injili wanaishi?
Tembelea Tovuti hii: https://joshuaproject.net/resources/articles/10_40_window



## Hebu natusikie kutoka kwako

Je, una maswali kuhusu somo la toleo hili au mada zingine za kimisheni? Masomo gani ungependa AfrikaTWENDE iyashughulikie? Tunakaribisha mawazo yako ili kulifanya gazeti letu kwenda na wakati na kubeba mada nyingi. Kwa maswali na maoni, tafadhali wasiliana nasi kwa baruapepe: afrikatwende@afrigo.org.

## Mtandao wa Maombi wa MANI

Wanachama wa Harakati inayojulikana kama 'Movement for African National Initiatives (MANI) Strategic Prayer Network (SPN)' walikutana Nairobi, Kenya kutoka Novemba 6 hadi 10, 2018, ili kujadili muunganisho wa huduma za kupeleka Injili na mikakati ya maombi ya pamoja. Walithibitisha kwamba makanisa yanayoombea maeneo ambayo bado hayajafikiwa yatahitajika kuyafikia maeneo hayo. Ufahamu unazidi kukua kwamba watoto na vijana wanaweza kutumiwa na Mungu kuomba kwa ajili ya watu ambao bado hawajafikiwa na Injili. [Kusubiri taarifa kama vile watu wangapi walihudhuria, nchi gani, nani alikuwa mwezeshaji.]



# MAKUNDI YA WATU: GUJARATI

Wagujarati ni kundi la watu ambalo limetawanyika sana takriban katika mataifa 129 na wanajumuisha asilimia 33 ya Wahindi wote walioko ughaibuni kote duniani. Asili ya Wagujarati ni katika jimbo la Gujarat Magharibi mwa India, na lugha yao ni Gujarati. Wakiwa wamejulikana kwa karne nyingi kama wafanyabiashara na watu wanaosafiri sana baharini kwa ajili ya biashara, mara nyingi wao huwa watu wa kwanza kuhamia nchi zingine duniani. Wagujarati wanasifika kwa uwezo wao mkubwa wa kufanya biashara. Kuanzia kuwa na viduka vidogo kwenye kona za nyumba mpaka kuwa na maduka makubwa ya kuuza bidhaa za kila aina. Ustadi wa Wagujarati katika biashara unajulikana tangu zamani.

Wagujarati wametoa viongozi wakubwa duniani kama vile Mahatma Gandhi, mwanaharakati wa kihindi aliyeongoza harakati za uhuru wa India kutoka kwa Waingereza. Waziri Mkuu wa sasa, Narendra Modi pia anatoka jimbo la Gujarati.

Kwa mujibu wa sensa ya dini katika jimbo la Gujarati ya mwaka 2011, asilimia 88.5 ni Wahindu, asilimia 9.67 ni Waislamu na asilimia 0.52 ni Wakristo. Asilimia inayobakia ambayo ni ndogo chini ya 2, inachangiwa na dini za Sikhs, Budha na Wajain kwa pamoja.

Dini ya Kihindu, ambayo ndiyo dini kubwa nchini India, ni dini kongwe ambayo imekuwepo tangu miaka 3000 kabla ya kuzaliwa Kristo, na leo ni dini ya tatu kwa ukubwa duniani baada ya dini za Ukristo na Uislamu. Dini ya Kihindu ni mchanganyiko wa imani na falsafa, na inaamini uwepo wa miungu mingi inayofikia milioni 33. Baadhi ya wanazuoni wake, huiita dini hii 'njia ya milele'.

## Kwa mtazamo

- Wahindi wa Gujarati ni kundi la watu lililotawanyika sana, wakipatikana angalau katika nchi 129 kati ya nchi 190 zilizopo duniani.
- Wagujarati wamejaliwa kuwa na uwezo mkubwa katika biashara.
- Asilimia 88.5 ya Wagujarati ni Wahindu, ilhani wakristo ni asilimia dogo, kama vile 0.52.
- Kimsingi wafanyabiashara, huwa wamejiweka wazi sana katika kujichanganya na watu wengine, baadhi yao wakiwa Wakristo.

## Mwombe Mungu:

- Achochee upendo wa majirani wakristo kwa jamii ya Gujarati.
- Ageuze macho ya Wagujarati kutoka kwenye njia za upotovu wa milele na badala yake awafunulie njia, kweli na uzima – Yesu.
- Afungue macho watu waone Ukuu wa Kristo. Kama wahindu, waweze bila ubishi kumpokea Kristo, siyo kama mmoja wa miungu yao mingi. Pia, wasije wakatafsiri vibaya mwito wa kuzaliwa upya kama aina ya mtu kutokea tena kuwa kiumbe tofauti baada ya kufariki dunia bali wampokee kama Mwokozi pekee wa roho na waelewe kuzaliwa mara ya pili kwa ajili ya uzima wa milele.

SIM By Prayer

AFRICA INLAND MISSION


**AFRIKA TWENDE**: **email**: afrikatwende@afrigo.org **AFRIGO**: **email**: afrigo_english@sim.org **ALLONS-Y !** : **email**: redactrice@sim.org

**SIM East Africa**
Tel: 251 911 206 530
east-africa.office@sim.org

**SIM West Africa**
Tel: +233 30 222 5225
wamo.personnel@sim.org

**SIM Southern Africa**
Tel: +27 21 7153200
za.enquiries@sim.org

**AIM International**
amc.io@aimint.org
https://aimint.org/african-mobilization/